



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA ISMANI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA NA MADIWANI
KATIKA KATA KUMI NA MBILI (12) ZA TANZANIA BARA**

Zanzibar, 20 Aprili, 2026.

1. Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Ismani, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa. Nafasi hiyo ilitokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo tajwa, **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi** kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichotokea tarehe 25 Machi, 2026.
2. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, tumepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa tarehe 08 Aprili, 2026 kuhusu uwepo wa nafasi wazi za madiwani kumi na mbili (12) kwa Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zilitokana na vifo vya madiwani kumi na moja (11) kwa nyakati tofauti na diwani mmoja (1) kupoteza sifa za uanachama.

Jimbo na kata zenye nafasi wazi zimeoneshwa katika Jedwali Na.1 na Na.2. kama ifuatavyo: -

Jedwali Na. 1: Jimbo lenye nafasi wazi ya Ubunge

Mkoa	Halmashauri	Jimbo	Sababu ya Jimbo kuwa wazi
Iringa	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Ismani	Kifo



Jedwali Na. 2: Orodha ya Kata zenye nafasi wazi za Madiwani

Na.	Halmashauri	Kata	Sababu ya Kata kuwa wazi
1.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	Mzimuni	Kifo
2.	Halmashauri ya Manispaa ya Kahama	Zongomera	Kifo
3.	Halmashauri ya Mji Nzega	Itilo	Kifo
4.	Halmashauri ya Mji Tarime	Ketare	Kifo
5.	Halmashauri ya Mji Kasulu	Nyumbigwa	Kifo
6.	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Kala	Kifo
7.	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	Ziba	Kifo
8.	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Kamsisi	Kifo
9.	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	Nyamugali	Kifo
10.	Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru	Namasakata	Kifo
11.	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	Bwongera	Kupoteza sifa za uanachama
12.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Kibiti	Kifo

3. Hivyo, kutokana na uwepo wa nafasi hizo wazi na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 49(1)(b), 49(2), 49(4), 61(1), 68(2) na 57(1) (a) na (b), (2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Sura ya 343, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu ratiba ya uchaguzi mdogo wa Ubunge Jimbo la Ismani, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa na Madiwani katika kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara kama ifuatavyo:


- i. Fomu za uteuzi kwa wagombea wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Madiwani katika Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara zitatolewa kuanzia tarehe **04 Mei, 2026 hadi 10 Mei, 2026;**
- ii. Uteuzi wa wagombea wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Madiwani katika Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara utafanyika tarehe **10 Mei, 2026;**




- iii. Kampeni za uchaguzi wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Madiwani katika Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara zitafanyika kuanzia **tarehe 11 Mei, 2026 hadi 31 Mei, 2026;**
- iv. Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Madiwani katika Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara utafanyika siku ya Jumatatu **tarehe 01 Juni, 2026.**

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na Maelekezo ya Tume katika kufanikisha ratiba ya Uchaguzi husika.

Imetolewa na:


Kailima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

